Serikali ilivyoandaa mazingira kuendeleza uvuvi

Na Stella Aron

UVUVI ni miongoni mwa sekta zenye mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Sekta hii huwezesha ajira, huchangia pato kwa taifa, huongeza vipato vya wavuvi pamoja na wadau wengine kama vile wachuuzi wa samaki na mazao mengine ya uvuvi, huongeza uhakika wa chakula na lishe.

Mbali ya hayo, inaposimamiwa kikamilifu vilevile huwezesha uhifadhi wa bionuai pamoja na utalii wa baharini, ziwani, mtoni na mabwawa.

Hapa nchini mchango wa sekta ya uvuvi kwa pato la taifa ni asilimia 1.7 kwa mwaka.

Pia hapa nchini sekta ya uvuvi hadi sasa huwezesha ajira kwa watu milioni 4.5, wakati upande wa lishe huchangia asilimia 30 ya protini.

Inakadiriwa kuwa, hapa nchini ulaji wa mazao ya uvuvi kwa mtu kwa mwaka ni kilo 8.5, kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na wastani wa ulaji wa samaki uliopendekezwa duniani, kilo 20.5.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashauri Ndaki, amesema kuwa Watanzania inabidi waongeze uzalishaji kwenye uvuvi, ili waongeze hata lishe inayotokana na mazao yake.

MAFANIKIO

Waziri Ndaki amesema kuwa, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uvuvi imetokana na usimamizi wa sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali iliyopo kwenye sekta.

Sera na sheria za uvuvi nchini ni pamoja na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015; Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003, Kanuni za Mwaka 2009 na Marekebisho ya Mwaka 2020; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Namba 29 ya Mwaka 1994; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Namba 11 ya Mwaka 2016; na Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi Bahari Kuu Namba 5 ya Mwaka 2020.

Waziri Ndaki amesema kuwa, sekta imefanikiwa kupunguza uvuviharamu na biasharaharamu za mazao ya uvuvi kwa asilimia 80 upande wa majibaridi, huku pia zikipunguzwa asilimia 100 za matumizi ya vilipuzi kwenye Ukanda wa Bahari ya Hindi.

Waziri anasema kuwa, mwaka 2020 jumla ya tani 497,567 za samaki wenye thamani shilingi trilioni 2.34 walivunwa ikilinganishwa na tani 362,645 samaki wenye thamani sh trilioni 1.48 mwaka 2015/2016.

Anasema kuwa, katika uzani huo, tani 435,408.9 ni samaki waliovunwa kwenye majibaridi, wakati tani 62,158.38 walivuliwa katika majichumvi kwa mwaka 2020, ikilinganishwa na tani 409,332.72 majibaridi na tani 60,976.51 majichumvi mwaka 2019.

Waziri anaendelea kusema kuwa, ongezeko la uvunaji wa rasilimali za uvuvi imetokana na kupungua vitendo vya uvuviharamu, kwamba ilikuwa ni mazingira yaliyowezesha kuongezeka mazalio ya samaki.

Anasema kuwa, vilevile mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 379 kwa miaka ya 2015 - 2017 hadi shilingi bilioni 691 miaka ya 2018/19.

"Hili ni ongezeko la asilimia 82. Aidha, uagizaji wa samaki kutoka nje ya nchi umepungua kwa asilimia 99.7, kutoka tani 22,962 zenye thamani ya sh. bilioni 56.12 mwaka 2016/17 hadi tani 8.21 zenye thamani ya sh. bilioni 0.16 mwaka 2020.

"Hii imesaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, kulinda soko la ndani, kuongeza ajira, na kupunguza urari wa kibiashara," Waziri Ndaki anasema.

Anasema kuwa mwaka 2020 vifaranga 21,676,187 vya samaki vilizalishwa, katika vituobinafsi (17,529,347) na serikali (4,146,840), ikilinganishwa na vifaranga 17,301,076 vilivyozalishwa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 25.3.

"Lengo ni kuzalisha vifaranga milioni 30 mwaka huu, ambapo vituo na taasisi za serikali vitazalisha vifaranga milioni 8, na sektabinafsi kuzalisha vifaranga milioni 22," anasema.

CHANGAMOTO

Akiwa katika moja ya mikutano iliyohusisha sekta ya uvuvi, waziri Ndaki alisema kuwa, kikao hicho kingeibua changamoto zinazoikabili.

Akitaja moja ya changamoto, alisema: "Nitaje tu baadhi ya changamoto ambazo wizara inakabiliana nazo.

"Changamoto hizo ni pamoja na mchango mdogo katika pato la taifa ikilinganishwa na rasilimali za uvuvi zilizopo nchini.

"Uvuviharamu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi, uwekezaji mdogo katika uvuvi wa baharikuu.

"Ukosefu wa bandari ya uvuvi, na kukosekana kwa meli za kitaifa katika uvuvi wa baharikuu."

Kuhusu ukuzaji viumbemaji, alitaja changamotokuu kwamba ni upatikanaji hafifu wa vifaranga na chakulabora cha samaki.

Pia, alitaja ufinyu wa huduma za ugani, kukosekana soko la uhakika, hususan kwa mazao ya mwani na kambale, pamoja na gharama kubwa za uanzishwaji shughuli za ukuzaji viumbemaji, hususan ufugaji samaki kwenye vizimba.

KUTATUA CHANGAMOTO

Waziri Ndaki anasema kuwa, serikali imedhamiria kuendeleza sekta ya uvuvi ili ichangie kikamilifu katika uchumi wa bluu, kwa misingi ya uvuviendelevu unaozingatia ikolojia na ustawi wa jamii.

"Hivyo, ili kufikia azma hiyo, serikali inatekeleza mikakati mbalimbali.

"Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na ujenzi wa bandari ya uvuvi, kufufua shirika la TAFICO, kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta ya uvuvi.

"Kuboresha tafiti zinazohusu rasilimali za uvuvi, kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi, kusimamia na kuendeleza shughuli za ukuzaji viumbemaji, na kuboresha huduma mbalimbali (mafunzo, ugani, maabara, ushauri na mazingira ya biashara ya mazao ya uvuvi)," anasema.

Anaendelea kusema kuwa, serikali inatekeleza mpango wa ujenzi wa bandari ya uvuvi ili kuboresha huduma kwa meli zinazofanya uvuvi wa kibiashara katika bahari, hususan Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu maarufu 'EEZ'.

Aidha, anasema kwamba ujenzi wa bandari ya uvuvi inakusudia uondoshe changamoto za kukosekana kwa huduma za kushusha samaki waliolengwa na wasiolengwa, ukaguzi wa samaki waliovuliwa, kuegesha na kufanya ukarabati wa meli, kupakia maji na chakula, mafuta, chambo, kushusha na kupakia mabaharia.

"Hatua zilizofikiwa katika ujenzi wa bandari ya uvuvi ni pamoja na kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa awali wa ujenzi wa bandari ya uvuvi kupitia mshauri muelekezi," anasema waziri.

Waziri Ndaki anasema kuwa pamoja na hayo, serikali inaendelea na mpango wa kufufua shirika la uvuvi Tanzania 'TAFICO', ambapo kazi mbalimbali zimefanyika, ikiwemo uandaaji wa mpangobiashara wenye maeneo matatu makubwa.

"Maeneo hayo ni uvuvi wa baharikuu, ufugaji samaki na uchakataji wa mazao ya uvuvi.

"Maeneo haya yatatekelezwa kupitia miradi midogo kumi yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 89.3, ikiwemo miradi ya uvuvi ya kununua meli nne za uvuvi 'long liner' na 'purse seiner';' mradi wa viwanda vya kuchakata samaki na miradi ya ukuzaji viumbemaji," anasema.

Anasema kuwa, serikali imepata ufadhili kutoka Serikali ya Japan kupitia Mpango wa Maendeleo ya Uchumi na Jamii (The Economic and Social Development Programme) wa fedha sh. bilioni 4.2, ambazo sehemu yake zitatumika kwa ujenzi wa meli yenye urefu wa mita 22, itakayovua kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari.

Aidha, anaendelea kusema kuwa, msaada huo itahusisha usimikaji mitambo ya kuzalisha barafu na ujenzi wa ghala ya ubaridi ya kuhifadhia samaki 'cold room'.

Waziri Ndaki anasema kuwa serikali inatarajia kuanza kutekeleza Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (IFAD).

Kwamba, programu hiyo imelenga kununua meli nane, ambazo nne zitakabidhiwa TAFICO, na nne nyingine Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO).

Akiizungumzia programu hiyo, anasema kwamba itajenga uwezo na kuendeleza vituo vya ukuzaji viumbemaji, itajenga kiwanda cha kuchakata samaki, itajenga kiwanda cha kutengeneza chakulabora cha samaki, na itaweka miundombinuwezeshi ya kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi.

"Serikali inaendelea kuhamasisha sektabinafsi ili kuwekeza katika uvuvi wa baharikuu," anasema.

Waziri Ndaki anasema kuwa, kuhusu ukuzaji viumbemaji na uzalishaji samaki kwenye mabwawa na vizimba, serikali imeazimia kujenga mazingirawezeshi kwa sektabinafsi kuwekeza katika shughuli mbalimbali za mnyororo wa thamani za mazao hayo, kuanzia uzalishaji wa mbegubora za viumbemaji, uzalishaji chakula, ukuzaji viumbemaji wa kibiashara, huduma za ugani, kuongeza thamani, usafirishaji na masoko.

"Ndugu washiriki, serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ili kuondoa changamoto zilizoainishwa, kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa viumbemaji kutoka tani 18,716.56 za sasa hadi kufikia tani 50,000 ifikapo mwaka 2025, na hatimaye tani 100,000 ifikapo mwaka 2030.

"Mikakati hiyo ni pamoja na kuanzisha vyama vya ushirika vya wafugaji wa samaki, ili waweze kukopesheka kwa urahisi.

"Kufanya kampeni za kuitambulisha tasnia ya ukuzaji viumbemaji kwenye taasisi za fedha, ili waweze kutoa dhamana na mikopo kwa wakuzaji viumbemaji.

"Kuanzisha atamizi za vijana kwa kutumia miundombinu itakayokuwepo katika vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbemaji,

"Na kuendelea kuhamasisha sektabinafsi kuwekeza katika vitotoleshi vya vifaranga vya samaki na viwanda vya chakula cha samaki," anataja.

WITO KWA WADAU

"Nitoe wito kwenu, tumieni fursa hii kuainisha changamoto zinazoikabili sekta hii, kuanzia ngazi ya mvuvi mmojammoja, vyama vya wavuvi, wachakataji wa samaki, na mazao yake, serikali na washirika wa maendeleo," amesema waziri.

Aidha, waziri Ndaki ametaka wadau watumie jukwaa ili kujadili changamoto hizo, na kisha wawasilishe mapendekezo wizarani kuhusu namna bora ya kuzipatia ufumbuzi.

"Vilevile, aimisheni wahusika na muda wa utatuzi wa changamoto hizo, kwa kuzingatia kuwa zipo changamoto ambazo utatuzi wake ni wa muda mfupi, wa kati na mrefu," anasema.

Ametoa wito kwamba wadau na sektabinafsi watumie fursa zilizoko za uwekezaji kwenye uvuvi baharikuu, uchakataji na biashara ya mazao ya uvuvi, ukuzaji viumbemaji, utengenezaji zana za uvuvi, utafiti, mafunzo, na utalii wa kiikolojia.

Amesema kuwa sekta ya uvuvi itaendelea kushirikishwa na sekta nyingine, ikiwemo mazingira, uchukuzi, viwanda na biashara, maliasili, utalii na nishati, ili kuhakikisha kwamba, usimamizi na matumizi ya rasilimali za uvuvi vinakuwa na tija na endelevu, hivyo kuongeza mchango wake kwa pato la taifa.

KAULI YA NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI

Akifunga mkutano wa wadau wa sekta ya uvuvi kwa mwaka 2021 uliofanyika kwa siku tatu kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Mwalimu Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul alisema kuwa, wadau wa sekta ya uvuvi nchini inatakiwa watumie fursa zinapojitokeza katika sekta hiyo, ili waweze kukuza uchumi, na kwamba wakati huohuo wakihakikishe wanakomesha uvuviharamu.

Naibu waziri Pauline alisema kuwa, kupitia mkutano wa wadau wa uvuvi, waliweza kuibua fursa mbalimbali zinazohusiana na uvuvi, hivyo kwamba wadau wakitumia vizuri fursa hizo, wataweza kunufaika.

"Moja ya fursa ambayo wameza kuibua ni pamoja na uwekezaji katika baharikuu.

"Tumeona TAFICO inavyokwenda kufufuliwa, pamoja na ujenzi wa bandari ya uvuvi Mbigani, Bagamoyo, pamoja na kununua meli nne, na kwa ujumla zinakuwa nane - na Zanzibar, kwa ajili ya kuanza uwekezaji katika baharikuu," naibu waziri Pauline.

Aidha, naibu waziri Pauline alisema kuwa, wameweza kufahamu mahitaji ya vyakula vya samaki, kwamba ni kiasi gani wajiandae kuelekea kwenye kilimo cha ufugaji wa samaki kwenye vizimba pamoja na mabwawa.

"Tunapoelekea kukuza sekta ya uvuvi, ni vizuri tukatumia fursa ya upatikanaji wa dhana bora ya uvuvi, ili kuweza kuwanufaisha wavuvi pamoja na wananchi kwa ujumla, na kuweza kukuza uchumi," amesema.

KATIBU MKUU

Katibu Mkuu Sekta ya Uvuvi, Dkt Rashid Tamatamah, amesema kuwa, siku za karibuni zilitokea taarifa kuhusu samaki kuonekana wamekufa kwenye maeneo mbalimbali ya Ziwa Victoria, na kwamba watu walipatwa hofu kuhusiana na uwezekano wa samaki hao kuingiwa sumu.

Katibu mkuu Dkt Tamatamah amesema kuwa, kutokana na taarifa hizo, hivyo wakatuma kikosi cha maabara kwa ajili ya kujiridhisha, na kwamba majibu yalipotoka ikaonekana samaki hao hawakuwa na sumu.

"Baada ya hofu kutokea, nilituma timu yangu ya maabara na kuchukua sampo ya samaki katika maeneo ya Rorya, Musoma, Mwanza, Sengerema na Bukoba.

"Tukazipeleka kwa mkemia mkuu, ili aweze kuangalia kama kuna sumu au wamekufa kwa mabadiliko ya tabianchi," Dkt Tamatamah anasema.

"Kuna hali huwa inajitokeza ziwani kwenye miezi ya baridi, ambayo inafanya maji ya juu kupata baridi na kuwa nyuzi joto sawa na yale ya chini.

"Hivyo, ikitokea upepo, maji ya chini yanakuja juu, na kuchanganyikana, na kusababisha baadhi ya samaki kufa."

Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda yeye ameshauri wastaafu na wale wanaotarajia kustaafu wasikubali kushindwa maisha, ila wajipe majukumubinafsi, ikiwemo ya ufugaji na ukulima.

"Usikubali kukaa tu nyumbani kuangalia TV na kucheza na wajukuu, utaondoka mapema sana.

"Kustaafu sio kuchoka, fanyeni kazi, wekezeni kwenye kilimo, wekezeni kwenye mifugo.

"Mimi nafuga nyuki, nalima, na pia ninajishughulisha na ufugaji wa samaki wa mabwawa," Pinda anasema.

Pinda anasema kuwa, wastaafu wengi wanaishi maisha ya tabu baada ya kustaafu, kwa sababu ya kukata tamaa kimaisha.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wengine, ikiwemo Dkt Christine Ishengoma (Mb); Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Almas Maige (Mb); Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Prof. Alexander Kitila Mkumbo (Mb); na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Uwekezaji).

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashauri Ndaki

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul

Scanned with CamScanner